

UTANGULIZI

Halmashauri ya walei: Uongozi wa Jumuiya, ni kijitabu maalumu kwa ajili ya kukumbusha juu ya utume wa walei kuendana na hati ya Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikano ‘Apostolicam Actuositatem’ ‘Harakati za Kitume’.

Hati hii imeidhinishwa na kuwekewa sahihi na Baba Mtakatifu Paulo wa Sita Askofu wa Roma na inatoa mwongozo juu ya nafasi na utume wa walei katika Kanisa.

Kwa sehemu ya kwanza ni wasilisho la hati hiyo iliyogawanywa katika sura sita. Katika sura hizo kutakuwa na uwasilishaji wa maana ya utume wa walei, kazi za kitume za walei katika makundi yao mbalimbali hasa kazi kubwa ikiwa ni kutakatifuza ulimwengu katika hadhi yao na kazi zao. Wanafanya utume huu wakishirikiana na makleri wao wanaowaongoza.

Na sehemu ya Pili ya kitabu ni wasilisho la mambo ya uongozi wa halmashauri ya walei katika ngazi ya Parokia, kigango, mtaa, shirikisho, jumuiya na mashirika ya kitume na utume mbalimbali katika kamati tendaji za parokia.

Sehemu ya tatu inahusu masomo ya kufatana na mazingira ya changamoto mbalimbali kubwa na ndogo zinazosibu jumuiya ndogondogo za kikristo.

Nawakaribisha nyote katika utumiaji wa kijitabu hiki kwa ajili ya ufahamu, weledi na maendeleo ya jumuiya ndogondogo na mashirika ya kitume katika utume wa walei.

Wenu katika Kristo
Rev. Fr. Mapendo Isidor